

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Anwani ya Simu: "ELIMU" Simu:
026 296 35 33
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz



Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S.L.P 10,
40479 DODOMA

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. GA.113/277/01/28

18 Februari, 2022.

Mwenyekiti,
TAMONGSCO,
S.L.P. 2662,
DODOMA

Katibu Mtendaji,
Christian Social Services Commission (CSSC),
S.L.P. 1454,
DAR ES SAALAM

Katibu Mtendaji,
Baraza la Waislam Tanzania (BAKWATA),
S.L.P. 21422,
DAR ES SAALAM

Mwenyekiti,
Tanzania Association of Private Inventors in Education (TAPIE),
S.L.P. 13346,
DAR ES SAALAM

Mwenyekiti
Baraza la Sunnah Tanzania (BASUTA),
S.L.P. 8581,
DAR ES SAALAM

Mkurugenzi,
Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET),
S.L.P. 13547,
DAR ES SALAAM.

WARAKA WA ELIMU NA.1 WA MWAKA 2022

KALENDA YA MIHULA KWA SHULE ZA AWALI, MSINGI NA SEKONDARI

MWAKA 2022

Tafadhali rejea kichwa cha habari.

2. Kutokana na changamoto zilizobainika katika utekelezaji wa Kalenda ya Mitaala ya Elimu kwa Shule za Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari nchini mwaka 2022, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeona kuna umuhimu wa kufafanua na kutoa maelekezo shirikishi ili kuweza kwa pamoja kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa awali wa Kalenda husika.

3. Katika muhtadha huo, Kalenda iliyoanza kutumika kuanzia tarehe 17/01/2022 itatumika kama Mwongozo wa Jumla katika utekelezaji wa Mitaala ya Elimu kwa ngazi hizo za elimu nchini.

4. Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule ambao ndio wasimamizi wakuu wa utekelezaji wa Kalenda ya Mitaala ya Elimu katika shule mbalimbali wanatakiwa kutekeleza mitaala kwa kuzingatia hali halisi na mazingira husika katika maeneo yao ili kuongeza tija katika ufundishaji na ujifunzaji na kuleta mafanikio ya kitaaluma nchini.

5. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia kwa Kamishna wa Elimu itaendelea kupokea maoni kutoka kwa wadau kwa nia ya kuboresha Kalenda ya utekelezaji wa Mitaala ya mwaka 2022.

Aidha, Kalenda ya Mihula ya Masomo kwa Shule za Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kwa mwaka 2022 itakuwa kama ifuatavyo:

MIHULA	KUFUNGUA MUHULA	LIKIZO FUPI		KUFUNGA MUHULA	IDADI YA SIKU ZA MASOMO
		KUFUNGA	KUFUNGUA		
Muhula I	17/01/2022	13/04/2022	19/04/2022	28/07/2022	131
Muhula II	05/09/2022	30/09/2022	10/10/2022	08/12/2022	63
Jumla ya Siku za Masomo					194

Tanbihi:

- Siku za Masomo kwa mwaka ni 194.
- Wanafunzi wote watapumzika kuanzia tarehe 29/07/2022 hadi 04/09/2022 kwa Muhula wa Kwanza ili kupisha Zoezi la Kitaifa la Sensa mwezi Agosti, 2022 na mwezi Disemba, 2022 watapumzika kwa Muhula wa Pili baada ya kufunga shule tarehe 08/12/2022.
- Mashindano ya UMITASHUMTA yatafanyika tarehe 30/07/2022 hadi 08/08/2022, na UMISSETA yatafanyika tarehe 09/08/2022 hadi 19/08/2022.
- Mashindano ya Michezo ya Shule za Sekondari za Afrika Mashariki (FEASSA) yatafanyika tarehe 10/09/2022 hadi 24/09/2022.

6. Waraka huu unaanza kutumika tarehe 18 Februari, 2022.

7. Nawatakiwa utekelezaji mwema.



Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
KAMISHNA WA ELIMU

Nakala: Wathibiti Wakuu Ubora wa Shule Kanda na Wilaya,
TANZANIA BARA.